

<p>Baba</p>		<p>Wakili</p>		<p>Mchungaji ya kondoo</p>		<p>Dereva wa Teksi</p>		<p>Mwalimu</p>	
<p>Mwanamuziki wa Kanisa</p>		<p>Mchungaji</p>		<p>Karani wa Duka</p>		<p>Daktari</p>		<p>Mpishi</p>	

<p>Mkusanya takataka</p>	<p>Mwalimu wa Shule ya Jumapili</p>	<p>Mama</p>
--------------------------	-------------------------------------	-------------

Fungu la Kumbukumbu

Yakobo 1:19 “Hayo mnejua, ndugu zangu wapenzi. Basi kila mtu na awe mwepesi wa kusika, bali si mwepesi wa kusema; wala kukasirika.”

Fungu la Kumbukumbu

Waefero 4:32 “ena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.”

Fungu la Kumbukumbu

2 Wakorintho 8:9 “Maana mnejua neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, jinsi alivyokuwa maskini kwa ajili yenu, ingawa alikuwa tajiri, ili kwamba ninyi mpate kuwa matajiri kwa umaskini wake.”

Fungu la Kumbukumbu

Yakobo 4:11 “Ndugu, msisingiziane; ansingiziane ndugu yake, au kumbukumu ndugu yake, husingizia sheria na kuihukumu sheria. Lakini ukihukumu sheria, huwi mtenda sheria, bali umekuwa hakimu.”

Fungu la Kumbukumbu

1 Petro 2:9 “Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu.”

Fungu la Kumbukumbu

Mathayo 19:26 “Yesu akawakazia macho, akawaambia, Kwa wanadamu hilo haliwezekani; bali kwa Mungu yote yawezekana.”

Fungu la Kumbukumbu

Luka 10:27 Akajibu akasema. Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote; na jirani yako kama nafsi yako.

Fungu la Kumbukumbu

Luka 6:38 “Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa; kipimo cha kujiaa na kushindiliwa, na kusukwa-sukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vitani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa.”

Fungu la Kumbukumbu

Yohana 8:12 “Basi Yesu akawaambia tena akasema, Mimi ndimi nuru ya ulimwengu, yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima.”

Fungu la Kumbukumbu

Waebrania 13:17 “Watiini wenye kuwaongoza, na kuwanyenyekea; maana wao wanakesha kwa ajili ya roho zenu, kama watu watakaotoa hesabu, ili kwamba wafanye hivyo kwa furaha wala si kwa kuugua; maana isingewataa ninyi.”

Fungu la Kumbukumbu

Kumbukumbu 31:8 “Naye BWANA, yeye ndiye atakayekutangulia, atakuwa pamoja nawe, hatakupungukia wala kukuacha; usiogope wala usifadhaike.”

Fungu la Kumbukumbu

Yohana 3:16 “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.”

Fungu la Kumbukumbu

Yohana 11:25 “Yesu akamwambia, Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi.”